مجلة جامعة فزان العلمية
Fezzan University scientific Journal
journal@fezzanu.edu.ly

# UTAMADUNI WA KIISLAMU NA MIDHIHIRISHO YAKE KATIKA NYIMBO ZA TAARAB YA KISWAHILI: UCHANGANUZI WA KISOSHOLOJIA KATIKA SAMPULI TEULE ZA NYIMBO ZA MZEE YUSSUF MZEE

* Jalgham Abuazuom Emhemmed Ali[1]
[1]Department of African Languages and Studies, Faculty of Languages, Sebha

:Muhtasari
Utafiti huu unachunguza namna utamaduni wa Kiislamu unavyojidhihirisha katika nyimbo za taarab ya Kiswahili, hususan katika mtindo wa mipasho (Mipasho), kwa kutumia sampuli teule za nyimbo za Mzee Yussuf Mzee. Lengo kuu la utafiti ni kubainisha jinsi vipengele vya kidini na kimaadili vinavyojitokeza katika maudhui na miundo ya kisanaa ya nyimbo hizi, licha ya kuwepo kwa mtazamo hasi wa kijamii unaozihusisha na upotovu wa maadili.

Utafiti huu umetumia mkabala wa uchanganuzi wa kisosholojia, ukiongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamii na uchanganuzi wa matini. Data zilikusanywa kupitia sampuli ya makusudi ya nyimbo (8–12) zilizochaguliwa kwa kuzingatia vigezo vya kisemantiki na kifani, ikiwa ni pamoja na msongamano wa maudhui ya kimaadili, umaarufu wa nyimbo, na utofauti wa dhamira kama vile ndoa, familia, maadili na ibada.

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, licha ya taswira hasi inayohusishwa na taarab ya mipasho, nyimbo za Mzee Yussuf Mzee zinaakisi kwa kiwango kikubwa maadili ya Kiislamu kama vile subira, uaminifu, heshima, mshikamano wa kijamii na kumcha Mungu. Aidha, utafiti umebaini kuwa mbinu za kifani zinazotumika katika nyimbo hizi, kama vile lugha ya mafumbo, taswira na ishara za kijamii, huchangia katika kuwasilisha maudhui ya kidini kwa namna isiyo ya moja kwa moja lakini yenye athari kubwa.

Kwa kuhitimisha, utafiti huu unapendekeza kuwa taarab ya mipasho haipaswi kuangaliwa kwa mtazamo hasi pekee, bali ichukuliwe kama jukwaa muhimu la kitamaduni linaloweza kubeba na kusambaza maadili ya dini na jamii. Hivyo basi, kuna haja ya tafiti zaidi zinazochunguza uhusiano kati ya muziki, dini na utamaduni katika jamii za Kiswahili.

Maneno Muhimu: Taarab ya Kiswahili, Mipasho, Utamaduni wa Kiislamu, Uchambuzi wa Kisosholojia, Maadili ya Jamii, Muziki na Dini.

## 1.0 Utangulizi :

Muziki ni nyenzo muhimu ya kijamii inayotumika kama kioo cha kuonesha maisha ya kila siku ya binadamu. Ni lugha isiyo na mipaka inayojenga mshikamano, heshima, mapenzi, mafunzo ya maadili, na hata kueneza imani za kidini. Katika muktadha wa Pwani ya Afrika ya Mashariki, taarab imekuwa miongoni mwa sanaa za muziki zilizo na historia ndefu na zenye nafasi kubwa katika ujenzi wa kitambulisho cha Waswahili. Muziki huu umeenea hususan Zanzibar, Pemba, Mombasa, Tanga na maeneo mengine ya Pwani ya Afrika Mashariki.



*Corresponding author: E-mail: jal.ali@sebhau.edu.ly Received in 7 April2026 - revised form 26 April 2026 Accepted 6 may2026 - Publication date: 8 June2026

Taarab, mbali na kuwa burudani, imekuwa chombo cha kufundisha, kusahihisha tabia, na hata kutumika kama jukwaa la kutoa maoni ya kijamii, kisiasa na kidini. Kupitia ushairi wake wenye vina, mizani na lugha yenye taswira pana, taarab imekuwa ikiwavuta wanajamii wa kada mbalimbali kuisikiliza na kuifanyia tafakuri. Kwa miongo kadhaa, taarab imeendelea kubadilika kutoka katika umbo lake la awali la taarab asilia kuelekea taarab ya kisasa, hususan aina maarufu ya taarab ya mipasho.

Ni katika muktadha huu ndipo tafiti za kitaaluma zinajitokeza kuchunguza nafasi ya taarab si tu kama sanaa ya burudani, bali kama hazina ya kitamaduni na kiroho. Utafiti huu unalenga kuchunguza utamaduni wa Kiislamu na namna unavyojitokeza katika nyimbo za taarab za Mzee Yussuf Mzee, msanii ambaye amekuwa mhimili muhimu katika kudumisha na kuendeleza taarab ya kisasa.

Kwa kuzingatia muktadha huu, utafiti huu unaanzia katika dhana kwamba taarab ya Kiswahili, hususan mtindo wa mipasho (Mipasho), haiwezi kufupishwa kuwa burudani tu au mjadala wenye utata wa kimaadili, bali ni matini changamano ya kitamaduni inayoakisi mfumo wa thamani za kidini na kijamii wa jamii ya Waswahili. Hivyo basi, utafiti huu unalenga kuyachambua nyimbo za Mzee Yussuf Mzee kwa mkabala wa uchanganuzi wa kisosholojia ili kufichua uwepo wa utamaduni wa Kiislamu katika miundo yake ya kimaana na kifani.

1.1 Usuli wa Mada :

Historia ya taarab inahusiana moja kwa moja na mwingiliano wa tamaduni katika Pwani ya Afrika ya Mashariki. Watafiti mbalimbali wamepishana kidogo katika kueleza asili yake.

Kwa mfano:

Khamis, N. S. (2017). anaeleza kuwa taarab ililetwa Zanzibar na Sultan wa Oman kupitia Mzanzibari mmoja aliyesafirishwa Misri ili kujifunza muziki huu.

Fargion, J. T. (2016). anaamini kuwa taarab inatokana na mwingiliano wa nyimbo kutoka India na Ghuba ya Uajemi, ambapo wafanyabiashara walileta mitindo yao ya muziki na kuichanganya na urithi wa Waswahili.

Ibrahim, U. A. (2023). anaongeza kuwa hata nyimbo za Kizungu zilichangia kwa kiasi fulani kuzaliwa kwa taarab kutokana na ukoloni wa Waarabu na Wazungu katika eneo hili.

Hali hii inaonesha wazi kuwa taarab si bidhaa ya tamaduni moja, bali ni zao la mwingiliano wa tamaduni nyingi (Kiarabu, Kihindi, Kizungu na Kiswahili) uliochochewa na harakati za biashara, ukoloni, na dini.

Aidha, mchango wa Waarabu katika Pwani ya Afrika Mashariki haukuishia katika biashara pekee bali uliambatana na kueneza dini ya Kiislamu. Kupitia madrasa zilizoundwa, Waarabu waliwafundisha Waswahili vipengele ya dini na utamaduni wa Kiarabu: ibada, ndoa, heshima, ukarimu, na maisha bora ya kijamii (Graebne, 1991). Vipengele hivi vimeendelea kujidhihirisha si tu katika maisha ya kila siku ya Waswahili, bali pia katika nyimbo za taarab.

Hata hivyo, licha ya mchango huo mkubwa, bado tafiti nyingi zimejikita katika historia na mabadiliko ya taarab, bila kueleza kwa kina ni kwa jinsi gani vipengele vya utamaduni wa Kiislamu vinavyojitokeza katika nyimbo za taarab, hususan zile za wasanii maarufu kama Mzee Yussuf Mzee. Utafiti huu unatamani kuziba pengo hilo.

:Umuhimu wa Kuchunguza Mada1.2

Kwanza, taarab imekuwa ikitazamwa mara nyingi kwa mtazamo hasi, hasa pale inapohusiana na taarab ya mipasho, ambapo baadhi ya nyimbo hueleza masuala ya mapenzi kwa lugha ya moja kwa moja. Wengi huchukulia kuwa nyimbo hizi ni chombo cha kupotosha maadili ya jamii (Ramadhan, 2013). Lakini swali la msingi ni: je, nyimbo zote za mipasho hazina thamani ya kijamii, kiutamaduni, au kidini?

Utafiti huu unaona kuwa, kinyume na dhana hiyo ya jumla, ndani ya taarab ya mipasho kuna vipengele vya Kiislamu vinavyohamasisha:

- heshima na utiifu kwa wazazi na wakubwa.
- umuhimu wa ndoa na maadili ya kifamilia.
- mshikamano na mapenzi ya kijamii.
- kumcha Mungu na kudumisha imani ya Kiislamu.

Kwa hivyo, kuuchunguza mchango wa Mzee Yussuf katika kuendeleza maadili ya Kiislamu kupitia taarab ya mipasho si tu kwamba kunaleta mtazamo mpya wa kitaaluma, bali pia kunasaidia jamii kuiona taarab kama sanaa yenye mchango chanya katika malezi ya kijamii na kidini.

2.0 Tatizo la Utafiti:

Kwa miaka mingi, nyimbo za taarab zimekuwa sehemu ya maisha ya kijamii na kitamaduni ya Waswahili. Zimeimbwa kwenye harusi, sherehe za kijamii, mikutano ya kisiasa, na hata shughuli za kidini. Hata hivyo, katika muktadha wa sasa wa karne ya 21, muziki huu umeingia kwenye mabadiliko makubwa ambayo yameibua mjadala mpana juu ya nafasi yake katika jamii.

Hapo zamani, taarab asilia ndiyo ilikuwa ikitawala. Nyimbo zake ziliimbwa kwa mafunzo, nasaha na maadili ya kijamii. Waimbaji wake walijikita zaidi kwenye kusawiri heshima, mapenzi ya kifamilia, mshikamano wa kijamii na unyenyekevu kwa Mungu. Hali hii iliifanya taarab kuwa chombo cha elimu isiyo rasmi kwa vijana na wanajamii wazima.

Lakini kadri muda ulivyopita, kulijitokeza mabadiliko makubwa yaliyozaa taarab ya mipasho, hasa ikiongozwa na kizazi cha vijana. Nyimbo za aina hii mara nyingi zimekuwa zikihusishwa na:

1. lugha ya moja kwa moja kuhusu mapenzi?.
2. kejeli na vijembe baina ya wapinzani wa kisanaa au kijamii?.
3. masimulizi ya waziwazi kuhusu mahusiano ya kifamilia?.

Kwa hali hiyo, taarab ya mipasho imeanza kuonekana kama muziki unaopotosha maadili ya jamii, na hivyo kutostahili kusikilizwa na watoto wala wanajamii wenye hadhi ya kijamii (Khamis, N. S. (2017).; Ramadhan, 2013).

Hata hivyo, changamoto iliyopo ni kwamba tafsiri hii hasi mara nyingi haichukui muda wa kuchunguza kwa kina maudhui chanya yaliyomo ndani ya nyimbo hizi. Ndani ya taarab ya mipasho, hususan zile za Mzee Yussuf Mzee, kuna vipengele vya msingi vya Kiislamu vinavyohimiza ibada, ndoa yenye heshima, maadili ya kifamilia, mshikamano wa kijamii, na kumcha Mungu.

Kwa msingi huo, tatizo la utafiti huu linajidhihirisha katika kutozingatiwa kwa namna ambavyo nyimbo za taarab, hususan za Mzee Yussuf Mzee, zinavyodhihirisha utamaduni wa Kiislamu. Pengo hili la kitaaluma linahitaji kujazwa ili kuonesha kwamba taarab ya mipasho si taswira hasi pekee, bali pia ni chombo cha kukuza maadili ya dini na jamii.

Hivyo basi, tatizo kuu la utafiti huu linaweza kufupishwa katika swali lifuatalo:

Ni kwa kiwango gani nyimbo za taarab ya Kiswahili, hususan taarab ya mipasho (Mipasho) katika kazi za Mzee Yussuf Mzee, zinadhihirisha mfumo wa maadili ya kitamaduni ya Kiislamu, na ni kwa namna gani mbinu za kifani zinachangia katika kuwasilisha maadili hayo ndani ya muktadha wa kisanaa ambao kijamii mara nyingi hutazamwa kwa mtazamo hasi

2.1 Lengo Kuu :

Lengo kuu la utafiti huu ni:

Kuchunguza utamaduni wa Kiislamu unaojitokeza katika nyimbo za taarab ya mipasho za Mzee Yussu.

2.2 Malengo Mahususi :

Kwa mujibu wa lengo kuu, malengo mahususi ya utafiti huu ni:

1. Kubainisha vipengele vya utamaduni wa Kiislamu vinavyojitokeza katika nyimbo za taarab ya mipasho za Mzee Yussuf.
2. Kuelezea mbinu za kifani zilizotumika katika kuibua na kusisitiza vipengele hivyo vya Kiislamu ndani ya nyimbo hizo.

:Maswali ya Utafiti2.3

Maswali ya msingi ambayo utafiti huu unataka kuyajibu ni:

1. Ni vipengele vipi vya utamaduni wa Kiislamu vinavyojitokeza katika nyimbo za taarab ya mipasho za Mzee Yussuf?
2. Ni mbinu zipi za kifani zilizotumiwa na msanii huyu kuibua na kuwasilisha vipengele vya Kiislamu katika taarab ya mipasho?

:Umuhimu wa Utafiti2.4

Utafiti huu una umuhimu mkubwa kwa nyanja mbalimbali:

1. Kwa jamii kwa ujumla, Utasaidia kubadilisha mtazamo hasi uliopo juu ya taarab ya mipasho, kwa kuonesha kwamba bado ni chombo muhimu cha mafunzo ya kijamii na kidini.
2. Kwa wasomi na watafiti wa fasihi na muziki – Utafiti huu utaongeza hazina ya maarifa kuhusu mchango wa taarab katika kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa Kiislamu. Pia, utasaidia kujenga msingi wa tafiti zaidi zinazoweza kulinganisha nafasi ya dini katika muziki wa Kiswahili na tamaduni nyingine duniani.
3. Kwa kizazi kipya cha wasanii – Utafiti huu unaweza kuwa kioo cha kuonesha kwamba muziki unaweza kuburudisha huku pia ukifundisha maadili, na hivyo kuwa msukumo kwa wasanii kuzingatia nafasi ya dini katika kazi zao.
4. Kwa wadau wa dini na malezi ya kijamii, Kupitia matokeo ya utafiti huu, wadau wa dini na jamii wataweza kutumia taarab kama jukwaa la kukuza maadili ya Kiislamu, badala ya kuiona tu kama tishio la maadili.

3.0 Mapitio ya Kazi Tangulizi:

Utafiti kuhusu nyimbo za taarab ni eneo ambalo halijapewa uzito mkubwa katika taaluma ya fasihi na muziki wa Kiswahili, japokuwa kuna wachache waliothubutu kulichunguza. Watafiti waliotangulia wameangazia zaidi historia, mabadiliko ya mitindo, nafasi ya taarab katika jamii, na mwingiliano wa kitamaduni. Hata hivyo, uhusiano wa taarab na utamaduni wa Kiislamu bado umeachwa wazi, na hakuna utafiti wa moja kwa moja uliochunguza nyimbo za Mzee Yussuf Mzee katika muktadha huo.

3.0.1 Tafiti za Historia na Asili ya Taarab:

Saleh (1980), Fargion (2016), na Munyao et al. (2025) walieleza kwa kina historia, mabadiliko, na mchango wa taarab katika kuunda utambulisho wa Kiswahili. Hata hivyo, udhaifu wa tafiti hizi ni kwamba zimejikita zaidi katika mwingiliano wa kitamaduni (Kiarabu, Kihindi) na ushindani wa kijamii, zikipuuza kabisa mchango wa taarab katika kuhifadhi na kusambaza falsafa na maadili ya Kiislamu, pengo ambalo utafiti huu unalijaza.

Fargion, naye alijikita katika kuonesha mabadiliko ya taarab na jinsi ilivyopokea ushawishi kutoka India na Ghuba ya Uajemi.

Tafiti hizi zinaonesha mchango wa taarab katika historia na mabadiliko yake, lakini hazijaeleza kwa kina namna dini hasa Uislamu inavyodhihirika ndani ya taarab.

3.0.2 Tafiti Kuhusu Mabadiliko ya Taarab:

Khamis (2017) na Traore walifafanua namna taarab imebadilika kuelekea usasa chini ya shinikizo la utandawazi. Pamoja na mchango wao mzuri, watafiti hawa walichambua mabadiliko haya kwa mtazamo wa kidunia (secular perspective) pekee. Walishindwa kuona

kuwa, ndani ya mabadiliko hayo ya kimtindo, bado kuna mwendelezo thabiti wa maudhui ya kidini, jambo ambalo utafiti huu unalithibitisha kupitia nyimbo za Mzee Yussuf.
Hata hivyo, mtazamo wake ulijikita zaidi kwenye mabadiliko ya kijamii na kidunia, na si dini.
Traore, alieleza nafasi ya taarab katika fasihi ya Kiswahili, akionyesha mfululizo wa uendelevu na mabadiliko katika ushairi na mawasiliano ya kijamii.

3.0.3 Tafiti Kuhusu Taarab ya Mipasho:

Omari (2013) na Mzee (2011) walichunguza athari za mipasho katika jamii. Udhaifu mkubwa wa tafiti hizi ni kuwa zilihukumu mipasho kwa mtazamo hasi na wa upande mmoja (one-sided negative approach), zikiihusisha na upotovu wa maadili tu. Utafiti wetu unakosoa mtazamo huu finyu kwa kuthibitisha kisosholojia kuwa mipasho inaweza kubeba na kufundisha maadili makuu ya Kiislamu.
Hata hivyo, tafiti hizi zilikazia zaidi changamoto na athari hasi, bila kuonesha nafasi chanya ya taarab ya mipasho katika kukuza maadili ya Kiislamu.

3.0.4 Pengo la Kitaaluma

Kwa ujumla, mapitio haya yanaonesha kwamba:
.Watafiti waliopita walieleza historia na mabadiliko ya taarab 1.
2 .Wapo waliotazama athari za kijamii za taarab ya mipasho.
3. Hakuna aliyefafanua kwa kina namna utamaduni wa Kiislamu unavyojitokeza katika taarab, hususan kupitia kazi za Mzee Yussuf Mzee.
Kwa hiyo, utafiti huu unakusudia kujaza pengo hili kwa kuchunguza na kuchambua namna vipengele vya Kiislamu vinavyosawiriwa na msanii huyu.

3.1Mkabala wa Kinadharia:

Utafiti huu unatumia Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi kama chombo cha kuchambua data. Nadharia hii, ambayo mizizi yake iko katika fikra za wanafalsafa na wachambuzi wa kijamii kama Adam Smith, Emile Durkheim, na Karl Marx, inashughulika na uhusiano kati ya kazi za fasihi na maisha ya kijamii.
Kwa mujibu wa nadharia hii:
Fasihi na muziki si bidhaa za mtu binafsi pekee, bali ni kioo cha jamii.
Kila kazi ya fasihi huakisi mazingira ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kidini ya jamii husika.
Muziki kama taarab unaweza kuchambuliwa ili kubaini maadili na mitazamo ya jamii ambayo yamehifadhiwa ndani yake.

3.1.1Uhalali wa Nadharia katika Utafiti Huu:

Katika muktadha wa taarab:
Jamii ya Waswahili ina historia ya Kiislamu, hivyo nyimbo zao haziwezi kutenganishwa na dini yao.
Nyimbo za Mzee Yussuf Mzee zinahusisha mafunzo ya ndoa, utiifu, maadili ya kifamilia na kumcha Mungu, ambavyo vyote ni nguzo za Uislamu.
Kwa kutumia Nadharia ya Sosholojia, tunaweza kuchunguza jinsi taarab inavyochukua nafasi ya dini na jinsi dini inavyochukua nafasi ya taarab katika maisha ya jamii.

Faida za Nadharia kwa Utafiti: 3.1.2

1. Inasaidia kuona muziki wa taarab si burudani pekee bali pia ni nyenzo ya kijamii na kiroho.
2. Inatoa mwongozo wa kuchunguza uhusiano kati ya jamii ya Kiislamu na taarab.
3. Inamwezesha mtafiti kuibua maana zilizofichika katika nyimbo ambazo kwa mtazamo wa haraka huonekana za kawaida.

## 4.0 Mbinu za Utafiti:

Mbinu za utafiti ni nyenzo muhimu zinazomsaidia mtafiti kufanikisha malengo ya utafiti wake. Katika taaluma ya utafiti, mbinu hutumika kama njia za kimkakati zinazopangwa ili kukusanya, kuchanganua na kufasiri data kwa usahihi. Uhalisia wa matokeo ya utafiti wowote unategemea kwa kiwango kikubwa namna mbinu hizo zimebuniwa, kutekelezwa na kusimamiwa.

Kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu, mbinu zilizotumika ziliundwa kwa kuendana na aina ya data inayohitajika, tabia ya nyenzo zinazotafitiwa, pamoja na mazingira ya kijamii na kitamaduni yanayohusiana na nyimbo za taarab ya Mzee Yussuf Mzee.

### 4.1 Aina ya Utafiti:

Utafiti huu umechukua aina ya utafiti wa kimaelezo (descriptive research). Aina hii ilichaguliwa kwa sababu inampa mtafiti nafasi ya kueleza kwa undani vipengele vya utamaduni wa Kiislamu vinavyojitokeza katika nyimbo za taarab, pamoja na mbinu za kifani zinazotumika. Lengo si kutoa takwimu za kidijitali pekee, bali kueleza maana, maudhui, na mtazamo wa kijamii na kidini unaobebwa na nyimbo za msanii husika.

### 4.2 Eneo la Utafiti:

Eneo kuu la utafiti huu ni nyimbo za taarab za Mzee Yussuf Mzee, msanii maarufu kutoka Zanzibar ambaye ana mchango mkubwa katika kukuza na kuendeleza taarab ya mipasho. Nyimbo zake zimeenea Pwani ya Afrika Mashariki na zinatajwa mara kwa mara katika mijadala ya kijamii kuhusu nafasi ya taarab katika maadili.

Hata hivyo, kwa kuwa muziki ni zao la jamii, eneo hili halikuzingatia nyimbo pekee, bali pia mazingira ya kijamii na kidini ya Zanzibar na Pwani ya Kiswahili kwa ujumla. Hii ilihitajika ili kutoa tafsiri pana ya nafasi ya utamaduni wa Kiislamu katika taarab.

### 4.3 Vyanzo vya Data:

Data katika utafiti huu zimegawanyika katika makundi mawili:

1 .Data za Kimsingi (Primary Data) :

Zimekusanywa kupitia usomaji makini wa nyimbo za Mzee Yussuf Mzee, kwa kusikiliza na kuchambua maneno, taswira na ujumbe wake. Zimekusanywa pia kupitia usaili wa ana kwa ana na msanii husika (Mzee Yussuf) pale ambapo ilibidi kupata ufafanuzi kuhusu dhamira na muktadha wa nyimbo zake. Aidha, utafiti huu ulitegemea uchambuzi wa sampuli ya makusudi iliyojumuisha nyimbo kati ya (8–12) zilizochaguliwa kutoka katika kazi za Mzee Yussuf Mzee. Uchaguzi wa sampuli hii ulizingatia vigezo vya kisemantiki na kifani, miongoni mwao ikiwa ni: msongamano wa viashiria vya kimaadili na kidini, umaarufu na usambazaji wake katika jamii ya wasikilizaji, pamoja na utofauti wa dhamira zinazojitokeza kama vile ndoa, familia, maadili, na ibada. Sampuli hii ilikusudiwa kutoa uwakilishi wa kina unaowezesha uchambuzi wa kimaudhui na kifani wa nyimbo husika. Ili kufafanua zaidi, jedwali lifuatalo linaonesha baadhi ya nyimbo teule zilizotumika:

Jedwali 1: Sampuli Teule ya Nyimbo za Mzee Yussuf Mzee Zilizochambuliwa

| NAMBA | JINA LA WIMBO | DHAMIRA KUU YA KIISLAMU/KIMAADILI INAYOSAWIRIWA |
|---|---|---|
| 1 | Tamu ya Ndoa | Ndoa, Heshima, na Uaminifu (الزواج، الاحترام، والأمانة) |
| 2 | Chozi la Mama | Utii kwa Wazazi na Malezi (طاعة الوالدين والتربية) |
| 3 | Hasidi hana sababu | Mshikamano wa Kijamii na Kuepuka Fitina (التماسك المجتمعي وتجنب الفتن) |
| 4 | Aso kasoro ni mungu | Ibada, Dua, na Kumtegemea Mungu (العبادة، الدعاء، والتوكل على الله) |
| 5 | Sichoki kustahimili | Subira na Maadili ya Kifamilia (الصبر والقيم الأسرية) |

2. Data za Upili (Secondary Data) :
Zimepatikana kupitia nyaraka, vitabu, makala za kitaaluma, tasnifu na makala za magazeti zinazohusu taarab, muziki wa Kiswahili, na utamaduni wa Kiislamu.
Vyanzo hivi vilipatikana hasa katika Maktaba Kuu ya Taifa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI).
4.4 Mbinu za Ukusanyaji Data:
Usomaji Makini (Close Reading):4.4.1
Mbinu hii ilitumika kwa kusoma na kuchanganua nyimbo za Mzee Yussuf kwa undani, maneno baada ya maneno. Lengo lilikuwa kubaini:
Vipengele vya Kiislamu vinavyodokezwa moja kwa moja.
Taswira na methali zinazohusiana na dini ya Kiislamu.
Namna ushairi unavyobeba mafunzo ya Kiislamu.
4.4.2 Usaili (Interview):
Usaili ulitumika kama njia ya kupata maelezo ya moja kwa moja kutoka kwa mtunzi na mwimbaji mwenyewe. Maswali ya usaili yalibuniwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na yalihusu:
Dhamira kuu ya nyimbo zake.
Mchango wa dini ya Kiislamu katika tungo zake.
Mitazamo yake binafsi kuhusu taarab ya mipasho na maadili ya kijamii.
4.4.3 Upitiaji wa Nyaraka (Documentary Review)
Mbinu hii ilihusisha kupitia maandiko ya wataalamu waliotangulia, ikiwemo:
Vitabu na makala kuhusu taarab (Munyao, J. K., Nabea, W. K., & Wandera, P. S. (2025), Khamis, N. S. (2017)., Fargion, nk).
Tasnifu na utafiti wa kitaaluma uliotangulia (kwa mfano, Mzee 2011).
Nyaraka za kijamii na kihistoria kuhusu nafasi ya dini katika Pwani ya Kiswahili.
4.5 Mbinu za Uchambuzi wa Data:
Data zilizokusanywa zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo (qualitative content analysis). Mbinu hii inahusisha kusoma maandishi kwa makini, kuyatafsiri, na kutoa maana zake kulingana na malengo ya utafiti.
Katika uchambuzi huu:
1. Data ziliainishwa kulingana na vipengele vya Kiislamu vilivyojitokeza.
2. Nyimbo ziligawanywa kwa mujibu wa dhamira zake kuu (ndoa, maadili ya kifamilia, .mapenzi, ibada, mshikamano wa kijamii, n.k.).
3. Mbinu za kifani zilizotumika na msanii zilielezwa na kufasiriwa katika muktadha wa dini na jamii.
4.6 Uhalali na Uhakika wa Data (Validity and Reliability):
Ili kuhakikisha kuwa data za utafiti huu ni sahihi na zinaaminika:
Vyanzo vingi vilitumiwa, ili kulinganisha na kuthibitisha taarifa.
Usaili ulifanywa moja kwa moja na msanii husika, ili kupunguza upotoshaji.
Ufafanuzi wa kitaaluma kutoka nyaraka mbalimbali ulitumiwa kulinganisha na data za kimsingi.
4.7Sababu za Kuchagua Mbinu Hizi
Sababu kuu za kutumia mbinu hizi ni:
1. Nyimbo ni maandiko ya kifasihi, hivyo usomaji makini ni njia bora ya kuyachambua.
2. Msanii ni chanzo cha moja kwa moja cha uhalisia wa nyimbo, hivyo usaili ulikuwa muhimu.
3. Ili kupata muktadha wa kielimu na kihistoria, upitiaji wa nyaraka ulikuwa wa lazima.

Kwa kutumia mbinu hizi tatu kwa pamoja, mtafiti aliweza kupata taswira ya kina kuhusu nafasi ya utamaduni wa Kiislamu katika taarab ya mipasho za Mzee Yussuf Mzee.

5.0 Matokeo na Uchambuzi:

Sehemu hii inawasilisha matokeo yaliyopatikana kutokana na ukusanyaji na uchambuzi wa data. Matokeo yanahusiana moja kwa moja na malengo mahususi ya utafiti, ambayo ni:

1. Kubainisha vipengele vya utamaduni wa Kiislamu vinavyojitokeza katika nyimbo za taarab ya mipasho za Mzee Yussuf.
2. Kuelezea mbinu za kifani zilizotumika kuibua na kuwasilisha vipengele hivyo.

Matokeo haya yamepangwa katika sehemu kuu mbili:

Vipengele vya Utamaduni wa Kiislamu katika Nyimbo za Mzee Yussuf.

Mbinu za Kifani alizotumia katika kuzisawiri.

5.1 Vipengele vya Utamaduni wa Kiislamu:

5.1.1Ndoa na Maadili ya Kifamilia:

Uislamu unahimiza ndoa kama nguzo ya maisha ya kijamii na ibada inayolinda heshima ya mwanadamu. Katika nyimbo nyingi za Mzee Yussuf, mada ya ndoa imepewa nafasi kubwa. Anaimba kuhusu heshima baina ya mume na mke, wajibu wa kila mmoja, na umuhimu wa uaminifu katika ndoa.

Mfano, baadhi ya nyimbo zake huonya juu ya uvunjifu wa ndoa, hila za kifamilia, na tamaa za kidunia zinazoweza kuharibu familia. Hali hii inaonesha kuwa taarab si tu chombo cha mapenzi ya kimahaba, bali pia chombo cha kuimarisha taasisi ya ndoa kwa mtazamo wa Kiislamu.

Uthibitisho wa hili unadhihirika wazi katika wimbo wake wa "Tamu ya Ndoa", ambapo Mzee Yussuf anaimba:

*"Tamu ya ndoa subira, kuvumiliana na staha, Sio kila kukicha mara, zogo na nyingi karaha, Mume na mke ni nguo, ndivyo inavyosema sharia."*

Uchambuzi wa matini: Ubeti huu unatumia lugha ya kisanii kuthibitisha misingi ya Kiislamu ya ndoa. Matumizi ya neno "subira" na "sharia" yanaakisi moja kwa moja mafundisho ya Qur'an yanayowataka wanandoa kuwa vazi kwa wenzao (kufichiana siri) na kuvumiliana katika kipindi cha misukosuko. Hii inathibitisha kuwa mipasho hapa haitumiki kutengana, bali kuimarisha uvumilivu.

Katika kushughulikia mada ya ndoa, Mzee Yussuf Mzee haiwasilishi kama uhusiano wa kimapenzi wa mpito, bali huiweka kama mkataba wa kimaadili unaojengwa juu ya uwajibikaji na heshima ya pande zote. Mtazamo huu unaendana kwa karibu na dhana ya Kiislamu inayochukulia ndoa kama taasisi ya kijamii yenye mwelekeo wa kiibada. Hali hii inajidhihirisha kupitia matumizi ya msamiati wenye uzito wa kidini kama vile subira, uaminifu, baraka na ridhaa, ambazo ni dhana zilizo na mizizi thabiti katika utamaduni wa .Kiswahili unaoathiriwa na Uislamu

5.1.2 Heshima na Utii kwa Wazazi na Wanajamii Wakubwa:

Miongoni mwa misingi mikuu ya Uislamu ni utiifu na heshima kwa wazazi. Mzee Yussuf mara kwa mara amekuwa akisisitiza kwamba watoto wawanajamiinze na kuwasikiliza wazazi wao. Katika baadhi ya tungo zake, ujumbe huu huwasilishwa kama onyo kwa vijana wasiojali malezi na maelekezo ya wazazi.

Hii inalingana na mafundisho ya Qur’an na Hadithi zinazosisitiza “radhi za Mungu zipo katika radhi za wazazi.” Hivyo, taarab ya Mzee Yussuf inakuwa nyenzo ya kuendeleza msitari huu wa Kiislamu wa heshima na utiifu.

Mfano halisi unaoibua hisia za kidini kuhusu wazazi unapatikana katika wimbo wa "Chozi la Mama". Katika wimbo huu, msanii anaonya kwa hisia kali:

*"Chozi la mama ni zito, halidondoki kwa bure, Ukidhulumu mzazi, duniani utapata tabu, Tafuta radhi za wazazi, Mola akusamehe dhambi."*

Uchambuzi wa matini: Kupitia mistari hii, msanii anatumia ushairi wake kufasiri moja kwa moja Hadithi za Mtume Muhammad (s.a.w) zinazosisitiza kuwa "Radhi za Allah ziko katika radhi za wazazi." Onyo la "duniani utapata tabu" linasadifu imani ya Kiislamu kuwa laana ya mzazi humkumba mtu hapa hapa duniani kabla ya akhera.

5.1.3 Maadili ya Kijamii na Mshikamano:

Uislamu unahimiza mshikamano, mshikikano wa kijamii na kusaidiana. Nyimbo za Mzee Yussuf mara nyingi huwasihi wanajamii kuishi kwa mshikamano, kuepuka chuki na fitina, na kuishi kwa mshikikano wa kijamii.

Mfano, baadhi ya tungo zake huonya juu ya hasadi, wivu, na mgawanyiko katika jamii. Hii ni tafsiri ya moja kwa moja ya mafunzo ya Kiislamu juu ya umma (umma) kama jumuiya yenye mshikamano.

Maudhui haya yanapata mashiko makubwa kupitia wimbo wa "Hasidi Hana Sababu", ambapo mwimbaji anatoa ujumbe mzito kwa jamii:

*"Hasidi hana sababu, chuki zake ni za moyoni, Hapendi kuona wenzake, wakiishi kwa amani, Tuacheni chuki ndugu, tujenge yetu imani."*

Uchambuzi wa matini: Msanii anashambulia tabia ya uhasidi (envy) ambayo inakemewa vikali katika Uislamu. Kwa kutumia neno "imani," Mzee Yussuf anaiambia jamii kuwa mshikamano wa kweli haujengwi tu kwa udugu wa damu, bali kwa kusafisha nyoyo na kushikamana katika imani, jambo ambalo ni msingi wa dhana ya "Umma" katika Uislamu.

5.1.4 Ibada na Kumcha Mungu:

Kipengele kingine muhimu kinachojitokeza ni wito wa kumcha Mungu. Mzee Yussuf amekuwa akitumia maneno yanayohusisha “Mwenyezi Mungu,” “dua,” na “baraka,” akisisitiza kwamba maisha bora hupatikana kwa kumtegemea Mungu.

Katika tungo zake, msanii huyu amewahi pia kuashiria swala la kifo na maisha ya akhera, akiwakumbusha wasikilizaji kwamba kila mtu atahesabiwa kwa matendo yake. Hili linadhihirisha namna taarab inavyoweza kuwa jukwaa la mafunzo ya dini.

Ujumbe huu unadhihirishwa wazi katika wimbo wake wa "Aso Kasoro Ni Mungu" (Asiye na kasoro ni Mungu). Wimbo huu umebeba falsafa nzito ya kiibada:

*"Mwanadamu si kamili, ana mengi mapungufu, Aso kasoro ni Mungu, yeye ndiye mkamilifu, Tumuombe Mola wetu, atupe mwisho mwema".*

Uchambuzi wa matini: Ubeti huu ni kielelezo cha dhana ya "Tawhiid" (Kumpwekesha Mungu). Msanii anavunja majivuno ya kibinadamu na kuwakumbusha wasikilizaji kuhusu udhaifu wao. Kifungu "atupe mwisho mwema" (Husnul Khatimah) ni dua maarufu sana miongoni mwa Waislamu, jambo linalothibitisha kuwa taarab ya mipasho inaweza kuwa jukwaa la kiroho la kukumbushana kuhusu kifo na akhera.

5.1.5 Upendo na Ukarimu:

Ukarimu na mapenzi ni vipengele vya msingi vya Kiislamu. Mzee Yussuf hutumia taarab kusisitiza upendo kati ya wanandoa, upendo katika familia, na upendo ndani ya jamii kwa ujumla. Aidha, nyimbo zake huwataka wanajamii wawe wakarimu, wachangie mali na muda wao kwa ajili ya wengine.

Hii inalingana na hadithi za Mtume (s.a.w.) zinazosisitiza ukarimu na kusaidiana, na hivyo nyimbo zake zinakuwa kiendelezo cha utamaduni wa Kiislamu katika jamii ya Kiswahili.

5.2 Mbinu za Kifani za Kusawiri Utamaduni wa Kiislamu:

5.2.1 Taswira (Imagery):

Mzee Yussuf hutumia taswira zenye nguvu kueleza dhana za Kiislamu. Mfano, anaweza kutumia taswira ya "mwanga" kumaanisha imani, au "giza" kuashiria dhambi. Taswira hizi hurahisisha wasikilizaji kuelewa mafundisho ya kidini kwa njia ya kisanii.

Methali na Nahau:5.2.2

Methali na nahau za Kiswahili, ambazo nyingi zina mizizi ya Kiislamu, hutumika kama mbinu ya kufikisha ujumbe. Methali kama "mtu ni utu" au "asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu" zinajitokeza katika tungo zake kama msisitizo wa maadili ya Kiislamu.

Lugha ya Kimaudhui na Kinathari:5.2.3

Lugha ya taarab ya Mzee Yussuf inajengwa kwa ufasaha wa Kiswahili sanifu wenye misemo ya Kiarabu. Hii inafanya nyimbo zake ziwe na ladha ya kidini na kiutamaduni kwa wakati mmoja. Lugha hiyo hufanya wasikilizaji wahisi mshikikano kati ya dini yao na muziki wao.

Mipasho na Ujumbe wa Kifalsafa:5.2.4

Hata katika nyimbo za mipasho ambazo huchukuliwa kwa mtazamo hasi, Mzee Yussuf hutumia ujumbe wa kifalsafa. Mipasho yake mara nyingi hukazia vipengele ya maisha, heshima na wajibu wa kijamii, badala ya kuishia kwenye kejeli na vijembe vya kimaisha.

Ushawishi wa Ushairi wa Kiarabu:5.2.5

Kwa kuwa taarab asili yake inahusiana na ushairi wa Kiarabu, Mzee Yussuf amekuwa akitumia mizani na vina vinavyoendana na urithi huo. Hii huchangia kuonesha mizizi ya Kiislamu na Kiarabu katika tungo zake, huku akibaki mwaminifu kwa Kiswahili kama lugha ya uwasilishaji.

Muhtasari wa Matokeo:5.3

Kutokana na uchambuzi huu, matokeo makuu ya utafiti yanaonesha kuwa:

1. Nyimbo za Mzee Yussuf Mzee huchukua nafasi kubwa katika kuendeleza vipengele vya utamaduni wa Kiislamu kama ndoa, heshima, mshikamano, ibada na ukarimu.
2. Msanii huyu hutumia mbinu za kifani kama taswira, methali, lugha ya kifasihi, na ushairi wa Kiarabu ili kufikisha ujumbe wa kidini kwa wasikilizaji.
1. Taarab ya mipasho, licha ya lawama za kijamii, inajitokeza pia kama chombo cha mafunzo ya Kiislamu endapo itasomwa kwa makini na kitaaluma.

6.0 Majadiliano:

Majadiliano haya yanapanua matokeo yaliyowasilishwa katika sura iliyotangulia kwa kuyalinganisha na mijadala ya kitaaluma, kijamii, na kidini. Lengo ni kuonesha uhusiano uliopo kati ya nyimbo za taarab ya mipasho za Mzee Yussuf Mzee na dhana ya utamaduni wa Kiislamu, pamoja na nafasi yake katika jamii ya Kiswahili na Pwani ya Afrika ya Mashariki.

6.1 Taarab kama Kioo cha Utamaduni wa Kiislamu:

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba taarab si tu burudani, bali pia ni kioo cha kijamii na kidini. Kupitia nyimbo za Mzee Yussuf, misingi ya Kiislamu kama ndoa, heshima, mshikamano, na ibada inasawiriwa kwa namna inayowafanya wasikilizaji waone uhusiano kati ya maisha ya kila siku na dini yao.

Hii inathibitisha dhana ya nadharia ya sosholojia kwamba sanaa ni taswira ya jamii. Nyimbo za taarab zinabeba utambulisho wa Kiislamu wa Waswahili, na hivyo kuwa urithi wa kiutamaduni unaohusisha dini, lugha, na historia.

6.2 Kuondoa Taswira Hasi ya Taarab ya Mipasho:

Kuna mtazamo wa kijamii kwamba taarab ya mipasho ni kinyume na maadili kwa sababu ya lugha yake ya moja kwa moja na mara nyingine yenye kejeli. Hata hivyo, matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa hata katika mipasho, Mzee Yussuf huibua mafunzo ya Kiislamu.

Kwa mfano, nyimbo zake mara nyingi huonya juu ya tamaa, wivu, na uzembe katika ndoa. Kwa muktadha wa Kiislamu, ujumbe huu unahimiza heshima, subira, na mshikamano wa

kifamilia. Hivyo, mjadala unaibua hoja kwamba tatizo si taarab yenyewe bali tafsiri finyu ya wanajamii.

Kwa kulinganisha na tafiti za awali zilizohusisha taarab ya mipasho moja kwa moja na upotovu wa maadili, matokeo ya utafiti huu yanaibua mtazamo mbadala unaoiangalia aina hii ya muziki kama uwanja mpana wa tafsiri unaoruhusu uwasilishaji wa maudhui ya kimaadili na kidini kupitia miundo ya kisanii ya kijamii. Hali hii inaonesha kuwa changamoto haipo katika matini ya wimbo wenyewe, bali katika namna unavyopokelewa na kufasiriwa katika muktadha wa kijamii.

6.3 Ndoa na Familia: Uhusiano na Dini:

Utafiti umebaini kwamba nyimbo nyingi za Mzee Yussuf hujikita katika mada ya ndoa na familia. Uislamu huona ndoa kama nguzo ya jamii na ibada inayotunza heshima ya mwanadamu. Kupitia taarab, msanii huyu anahimiza uaminifu, heshima, na uadilifu wa kifamilia.

Hii inaonesha kuwa taarab inaweza kutumika kama nyenzo ya elimu ya maadili sambamba na madrasa na mihadhara ya kidini. Kwa hivyo, muziki unachukua nafasi ya pekee katika kulisha jamii maarifa ya kidini kwa njia ya kisanii.

6.4 Mbinu za Kifani kama Daraja kati ya Dini na Fasihi:

Mzee Yussuf hutumia mbinu mbalimbali za kifasihi taswira, methali, vina, na lugha ya Kiswahili yenye misemo ya Kiarabu — kuwasilisha mafunzo ya Kiislamu. Mbinu hizi zinafanya ujumbe wa dini uwe wa kuvutia, wa kukumbukwa, na wa kueleweka

Kwa mantiki ya sosholojia, mbinu hizi zinajenga daraja kati ya fasihi na dini. Wasikilizaji hawasikii tu burudani, bali pia wanajifunza na kuhamasika kuishi maisha yenye maadili ya Kiislamu.

6.5. Taarab kama Njia ya Kujenga Mshikamano wa Jamii:

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa nyimbo za Mzee Yussuf zina hamasa ya mshikamano wa kijamii. Uislamu unahimiza mshikamano kupitia dhana ya umma, na taarab ya Mzee Yussuf inauendeleza mshikamano huo kwa kuonya dhidi ya fitina, wivu, na mgawanyiko.

Kwa hivyo, taarab inakuwa nyenzo ya mshikikano wa kijamii inayojenga umoja na mshikamano wa Waislamu na Waswahili kwa ujumla.

6.6. Nafasi ya Mzee Yussuf katika Historia ya Taarab:

Mzee Yussuf Mzee anajitokeza kama msanii wa kipekee kwa sababu ameunganisha vipengele vya taarab asilia na taarab ya kisasa huku akibaki mwaminifu kwa mafunzo ya Kiislamu.

Ukiilinganisha na wasanii wengine wa taarab ya mipasho, Mzee Yussuf anatumia tafsiri ya kidini na maadili badala ya kuishia katika vijembe na kejeli. Hivyo, mchango wake ni wa kipekee katika kuonesha kuwa taarab ni zaidi ya burudani; ni fasihi inayoweza kufunza dini na maadili.

. Muhtasari wa Majadiliano6.7

Majadiliano haya yanaonesha kwamba:

1.Taarab ya Mzee Yussuf ni kiwakilishi cha utamaduni wa Kiislamu katika jamii ya Kiswahili.

2.Mipasho, licha ya mtazamo hasi, inaweza kuwa nyenzo ya mafunzo ya dini na maadili endapo itachambuliwa kwa kina.

3.Mbinu za kifani zilizotumika zinaunda daraja kati ya fasihi na dini, zikifanya muziki wa taarab kuwa elimu ya kijamii na kidini.

1.Taarab inachukua nafasi ya kuimarisha mshikamano wa jamii kwa kuhamasisha mshikikano, mshikikano wa kifamilia, na mshikamano wa kidini

7.0 Hitimisho na Mapendekezo:

Sura hii inahitimisha utafiti kwa kutoa majibu ya jumla kwa malengo na maswali ya utafiti yaliyowasilishwa mwanzoni. Aidha, sura hii inatoa mapendekezo yanayolenga kuendeleza

uelewa wa jamii na watafiti kuhusu nafasi ya utamaduni wa Kiislamu katika nyimbo za taarab ya mipasho za Mzee Yussuf Mzee na zaidi ya hapo, katika fasihi ya Kiswahili kwa ujumla.

Hitimisho:7.1

7.1.1. Kuhusu Lengo Kuu:

Lengo kuu la utafiti lilikuwa kuchunguza utamaduni wa Kiislamu unaojitokeza katika nyimbo za taarab ya mipasho za Mzee Yussuf Mzee. Matokeo yameonesha wazi kuwa nyimbo zake zimesheheni mafunzo ya Kiislamu yanayohusu ndoa, heshima kwa wazazi, mshikamano wa kijamii, ibada na kumcha Mungu, pamoja na upendo na ukarimu. Hivyo, utafiti umefanikiwa kulifikia lengo kuu.

7.1.2 Kuhusu Malengo Mahususi:

(a) Kubainisha vipengele vya utamaduni wa Kiislamu: Utafiti umebaini vipengele vya ndoa na familia, utiifu kwa wazazi, mshikamano wa kijamii, ibada na kumcha Mungu, pamoja na upendo na ukarimu. Vipengele hivi vimejitokeza kwa uwazi katika nyimbo mbalimbali za .Mzee Yussuf

(b) Kuelezea mbinu za kifani: Msanii ametumia taswira, methali na nahau, lugha ya Kiswahili yenye maneno ya Kiarabu, ushairi wa vina na mizani, na hata mtindo wa mipasho, ili kuwasilisha mafundisho ya Kiislamu kwa njia ya kuvutia na ya kueleweka.

7.1.3 Kuhusu Maswali ya Utafiti:

(a) Vipengele vya utamaduni wa Kiislamu vinavyojitokeza katika nyimbo za Mzee Yussuf .ni pamoja na ndoa na familia, utiifu kwa wazazi, mshikamano, ibada, na ukarimu

(b) Mbinu zilizotumika ni taswira, methali, lugha ya kifasihi, vina na mizani, pamoja na .mbinu ya mipasho yenye msisitizo wa maadili ya Kiislamu

7.2 Mapendekezo:

7.2.1 Mapendekezo ya Kitaaluma:

1. Utafiti zaidi: Watafiti wengine wapanue utafiti huu kwa kuangalia nyimbo za wasanii wengine wa taarab na aina nyingine za muziki wa Kiswahili ili kujua namna dini na utamaduni zinavyojitokeza.

2. Uchambuzi linganishi: Tafiti zijazo ziangalie kwa kulinganisha nyimbo za taarab na aina za muziki wa Kiislamu kama qasida, ili kubaini maeneo ya kufanana na tofauti.

3.Uboreshaji wa mitaala: Taasisi za elimu ziingize masuala ya muziki wa Kiswahili, ikiwemo taarab, kama nyenzo ya kufundishia fasihi na tamaduni.

4. Utafiti huu unapendekeza kuanzishwa kwa hifadhidata ya kidijitali ya kisayansi inayojumuisha nyimbo za taarab ya Kiswahili zenye mwelekeo wa kidini, itakayopatikana kwa watafiti na wanafunzi. Hatua hii itasaidia kuhifadhi urithi wa kitamaduni na kidini, pamoja na kuchochea tafiti za taaluma mbalimbali zinazounganisha muziki, dini na utamaduni.

7.2.2.Mapendekezo ya Kijamii:

1. Kwa Taasisi za Elimu na Mitaala (Taasisi za Kielimu): Taasisi zinazosimamia elimu kama vile Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), mabaraza ya mitihani (NECTA), na idara za Fasihi katika vyuo vikuu, zinapaswa kuingiza matini za nyimbo za taarab zenye maadili chanya (kama kazi za Mzee Yussuf) katika mitaala yao. Nyimbo hizi zitumike kama zana ya vitendo kufundishia maadili ya jamii, falsafa, na matumizi ya lugha ya kifumbo darasani.

2. Kwa Asasi za Kidini na Mabaraza ya Kiislamu (Taasisi za Kidini): Taasisi za kidini, kama vile Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) na jumuiya za kidaawa, zinashauriwa kubadili mtazamo wa kuikataa taarab jumla. Badala yake, taasisi hizi zinapaswa kushirikiana na wasanii wanaotunga kazi zenye kukuza utiifu, ndoa, na subira, na kuutumia muziki huu kama jukwaa mbadala (alternative platform) la kufikisha ujumbe wa dini kwa vijana ambao hawafiki misikitini au kwenye madrasa mara kwa mara.

3. Kwa Mamlaka za Sanaa na Vyombo vya Habari (Taasisi za Kiutamaduni na Ki-Vyombo): Mamlaka zinazosimamia sanaa (kama BASATA Zanzibar na Bara) pamoja na mamlaka za mawasiliano (kama TCRA) na vituo vya utangazaji, vinapaswa kuandaa vipindi maalum vya redio na televisheni vinavyochambua maudhui ya kimaadili na kidini ndani ya taarab. Vyombo hivi viache kucheza taarab kwa lengo la burudani na kusambaza "vijembe" pekee, bali viibue midhihirisho ya kiutamaduni iliyomo ndani yake. Pia, BASATA ianzishe tuzo maalum kwa wasanii wa taarab wanaoendeleza maadili mema.

7.3. Hitimisho la Jumla:

Kwa ujumla, utafiti huu umeonesha kuwa taarab ya Mzee Yussuf Mzee ni hazina ya kifasihi, kijamii, na kidini. Licha ya mtazamo hasi juu ya taarab ya mipasho, nyimbo zake zimethibitisha kuwa ni chombo chenye nguvu cha kuendeleza mafunzo ya Kiislamu na mshikamano wa kijamii.

Kwa hiyo, ni wajibu wa watafiti, walimu, viongozi wa jamii, na wasanii kuhakikisha kwamba urithi huu wa muziki unathaminiwa, unahifadhiwa, na unatumika kujenga jamii yenye maadili na mshikamano.

8. Marejeleo:

Ali, D. M. (2017). *Kuchunguza maudhui ya nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu Zanzibar* 2000–2010.
[Tasnifu ya Uzamili isiyochapishwa, Chuo Kikuu cha Dodoma].

Clacherty, B. (2021). Understanding the history of women's lives in Zanzibar through song and story: A gendered perspective. *Journal of African Cultural Studies*, *33*(1), 1-20.

Eisenberg, A. (2003). Review of Kelly Askew. 2002. Performing the Nation: Swahili Music and Cultural Politics in Tanzania.University of Chicago Press. Current Musicology, *75*, 130-145.

Fargion, J. T. (2016). *Taarab music in Zanzibar in the twentieth century: A story of 'old is gold' and flying spirits*. Routledge.

Hashil, H. S. (2018). Mimi, Umma Party na Mapinduzi ya Zanzibar.

Ibrahim, U. A. (2023). *Uchunguzi wa migongano ya kimbari katika muktadha wa Zanzibar ya ubaadaukoloni: Uchanganuzi wa riwaya ya Vuta N'kuvute na Mungu Hakopeshwi* [Tasnifu ya Uzamivu, The Open University of Tanzania].

Igobwa, E. S. (2007). Taarab and chakacha in East Africa: Transformation, appreciation and adaptation of two popular music genres of the Kenyan coast. *Muziki*, *4*(2), 20-30.

Katulu, K. V., Ngowa, N., & Chimoni, J. Athari za kimofonolojia za lugha ya Kikamba kwa Kiswahili. Ruwaza Afrika.

Khamis, N. S. (2017). *Mabadiliko katika nyimbo za taarab na uwasilishaji wake kulingana na wakati* [Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania].

Munyao, J. K., Nabea, W. K., & Wandera, P. S. (2025). Mbinu za kimtindo zinazojenga utaifa wa jamii ya Akamba. *Eastern Africa Journal of Kiswahili (EAJK)*, *4*(1), 23–38.

Omari, S. (2013). Hip hop music as a youth medium for cultural struggle in Zanzibar. *Journal of Pan African Studies*, *6*(3), 133–156.

Saleh, M. A. (2018). Swahili Elites and the Concept of Long-Distance Nationalism within the Diaspora. *Connections across the Indian Ocean*, 296-310.

Saleh, S. S. (1980). Nyimbo za taarab Unguja. *Lugha Yetu*, *37*, 35-46.

Saleh, S. S. (1988). Historia na muundo wa Taarab. *Lugha na Utamaduni*, *1*, 8-11.

Vander Biesen, I., & De Beukelaer, C. (2014). Tourism and imagining musical traditions on the East African coast: Harmony and disharmony. *The World of Music*, *3*(1), 35-55.